



# BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (NACTVET)



## JARIDA LA SEPTEMBER, 2024

TOLEO: 0001

TAREHE 30 SEPTEMBER, 2024

### NACTVET yawajengea uwezo Wamiliki na Wakuu wa Vyuo vya TVET Kanda ya Mashariki



Wamiliki na Wakuu wa Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi wameaswa kuzingatia misingi ya uongozi na utawala bora kama nguzo muhimu katika kuimarisha utoaji wa elimu bora ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi hapa nchini.

Rai hiyo imetolewa tarehe 26 Septemba, 2024 jijini Dar es Salaam na Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Dkt. Adolf Rutayuga, wakati wa ufunguzi wa warsha ya kuwajengea uwezo wamiliki, wajumbe wa Bodi, wakuu wa vyuo, na wasimamizi wa vyuo vilivyoko katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

Katika hotuba yake, Dkt. Rutayuga amesema kuwa maadili ni msingi wa kuaminika katika uendeshaji wa taasisi za elimu, na kuhimiza washiriki kuchukua hatua madhubuti katika kuhakikisha maadili na miongozo iliyowekwa na NACTVET inazingatiwa katika shughuli zao za kila siku.

Dkt. Rutayuga amebainisha wazi kuwa Serikali ya Tanzania imejizatiti kikamilifu kuimarisha ubora na upatikanaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TVET) nchini kote.

Dkt. Rutayuga ameangazia miongoni mwa mikakati ya kufanikisha jitihada hizo kuwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa uthibiti wa ubora wa TVET.



[www.nactvet.go.tz](http://www.nactvet.go.tz)

**"NACTVET - UJUZI, UBORA, UMAHIRI"**

nactvet







"Kama Baraza tunahakikisha kwamba mipango yetu ya kuwezesha utoaji mafunzo inakidhi viwango vya juu zaidi vya ubora. Tunaamini kwa kufanya kazi pamoja, tunaweza kuhakikisha kwamba mipango yetu ya mafunzo inawiana na mahitaji ya uchumi wetu, na hatimaye kuzalisha nguvu kazi inayoendana na mahitaji ya soko la ajira na kasi ya mabadiliko," amesema.



Lengo la warsha hiyo ni kujibu ombwe la uwezo wa mazingatio ya utawala, uongozi na maadili ndani ya vyuo vya TVET ili kuboresha utoaji mafunzo na kuzalisha wahitimu wenye ujuzi na umahiri, unaotakiwa na soko la ajira.

Warsha hiyo imetoa fursa kwa washiriki kubadilishana mawazo na kujifunza mbinu mbalimbali za kuboresha uongozi na utawala katika vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, ili kukabiliana na changamoto zinazokabili sekta ya elimu ya ufundi nchini.

Warsha imefanyika kwa siku mbili ambapo tarehe 26/09/2024 wahusika walikuwa ni Wamiliki na Wajumbe wa Bodi za Vyuo na tarehe 27/09/2024 ambapo walengwa walikuwa Wakuu wa Vyuo na Wasimamizi wa Vyuo.





## Waziri Mkenda afanya Mazungumzo na Mwenyekiti wa Baraza NACTVET



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amekutana na kufanya mazungumzo na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) Bi. Bernadetta Ndunguru ambaye alifika kwa ajili ya kujitambulisha jijini Dodoma tarehe 4 Septemba, 2024.

Katika kikao hicho Prof. Mkenda amesisitiza Bodi ya NACTVET kuendelea kuimarisha na kusimamia elimu ya Ufundi katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo Toleo la 2023 inayojielekeza katika elimu ujuzi.



Kwa upande wake Bi. Bernadetta Ndunguru amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa

kuaminiwa katika nafasi hiyo pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kuahidi kutekeleza jukumu la kusimamia na kuendeleza Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa ufanisi.



Ameongeza kuwa anafahamu vilio vya ajira nchini, hivyo jukumu mojawapo ni kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanawezesha wahitimu kupata maarifa na ujuzi utakaowawezesha kujijiri au kuajirika ndani na nje ya nchi.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Naibu Waziri Mhe. Omar Kipanga na Naibu Makatibu Wakuu Prof. Daniel Mushi na Dkt. Wilson Mahera.



# Maandalizi Utekelezaji wa Mradi wa ESPJ II Yaanza



Maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi Awamu ya pili (Education and Skills for Productive Jobs – ESPJ II) yameanza kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa elimu nchini. Mradi unalenga kufanya mabadiliko chanya katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuwawezesha wahitimu kupata ujuzi na umahiri wa kuweza kujajiri au kuajiriwa.



Mnamo tarehe 6 Septemba, 2024, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia anayeshughulikia Elimu, Dkt. Wilson Mahera, alihudhuria kikao cha tathmini ya maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa ESPJ II kilichofanyika katika ofisi za NACTVET Kanda ya Mashariki jijini Dar es Salaam.



Kikao hicho kilihusisha wadau mbalimbali wa elimu wanaotarajiwa kushiriki katika utekelezaji wa mradi huo hapa nchini wakiwemo wataalam kutoka Benki ya Dunia.



# NACTVET yashiriki Maadhimisho ya Siku ya Kitaifa ya Wahandisi



Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) limeshiriki Maadhimisho ya 21 ya Siku ya Wahandisi yaliyofanyika tarehe 5 hadi 6 Septemba, 2024 jijini Dar es Salaam.

Waziri wa Ujenzi, Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) alifungua rasmi maadhimisho hayo tarehe 5 Septemba, 2024 na kutoa wito wa Wahandisi kuhakikisha utekelezaji wa kazi zao unaendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia mbalimbali ikiwemo Akili Mnemba.



Mhe. Bashungwa alitembelea banda la NACTVET wakati wa maadhimisho hayo na kueleza juu ya shughuli zinazofanywa na Baraza hasa katika eneo la uthibiti ubora wa

elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuzalisha wahitimu wenye ujuzi.



Maadhimisho hayo yaliongozwa na Kauli Mbiu "Kuandaa Nguvukazi ya Uhandisi katika zama za Akili Mnemba: Mafunzo na Kuimarisha Ujuzi wa Wataalam wa Kanda ya Uhandisi" yalifungwa tarehe 6 Septemba, 2024 na Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Rahma Kassim Ali.



# Ujuzi Queens yajinoa Mashindano ya SHIMUTA



Timu ya Netiboli ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) Ujuzi Queens inaendelea kujinoa ikiwa ni maandalizi ya Mashindano ya Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni Binafsi (SHIMUTA) yanayotarajiwa kufanyika jijini Tanga mwezi Novemba, 2024.

Kapteni wa Timu ya Ujuzi Queens, Bi. Bernadeta Kipaya amesema timu hiyo inaendelea kujiimarisha kwa kufanya mazoezi mara kwa mara na kwamba washiriki wamejipanga vyema kung'ara kwenye mashindano hayo.

"Nafurahi kuona namna wanamichezo wanaweka juhudi katika maandalizi ya kuelekea mashindano ya SHIMUTA. Naamini timu yetu itafanya vizuri kwa kuwa kwa umoja wetu tumedhamiria kupata ushindi".





## **JE, WAJUA?**

**UNaweza KUOMBA NAMBA YA UTAMBULISHO WA TUZO (AVN) MARA TU BAADA YA MATOKEO YA DIPLOMA KUFANYIWA UHAKIKI.**

**"OMBA SASA, USISUBIRI MPAKA KIPINDI CHA UDAHILI"**



## **NAMNA YA KUOMBA AVN**

1. Bofya [www.nactvet.go.tz](http://www.nactvet.go.tz)
2. Bofya sehemu iliyoandikwa Request Award Verification Number kwenye key links
3. Jaza Taarifa zako kulingana na maelekezo
4. Fanya Malipo kwa kutumia Namba ya Malipo utakayopatiwa
5. Hifadhi Namba ya Tuzo utakayotumiwa kwa ajili ya kufanya Udahili katika chuo unachotaka kujiunga.

# IFAHAMU NACTVET

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) ni Taasisi iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge, Sura 129 na Marekebisho yake ya mwaka 2021 na kupewa jukumu la kusajili, kutoa ithibati, kuthibiti ubora na kuratibu utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi nchini.



+255 26 232 3121  
+255 733 777 751  
+255 736 310 311



P. O. Box 17007,  
NSSF Building - 3rd Floor,  
Mwangosi Road,  
41110 Kilimani, Dodoma.



[info@nactvet.go.tz](mailto:info@nactvet.go.tz)





[www.nactvet.go.tz](http://www.nactvet.go.tz)



nactvet

**"NACTVET - UJUZI, UBORA, UMAHIRI"**